**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI - TABORA

**S.L.P. 62, TABORA, TANZANIA**
**Simu: +255 (0) 26 2605058**
**Nukushi: +255 (0) 26 2605338**
**BaruaPepe:*info@bti.ac.tz***
**Tovuti*: www.bti.ac.tz***

Kumb. Na. B/TRA/I/VOL. IV/09 17/02/2017

## NAFASI ZA KUJIUNGA NA KOZI YA UFUGAJI NYUKI KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018

Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora kinatangaza nafasi za masomo kwa mwaka wa masomo 2017/2018 katika ngazi ya Stashahada na Astashahada.

**Kozi zinazotangazwa**

i. Astashahada ya Awali ya Ufugaji Nyuki: Mwaka mmoja (1) (NTA - Level 4)
ii. Astashahada ya Ufugaji Nyuki: Mwaka mmoja (1) (NTA - Level 5)
iii. Stashahada ya Ufugaji Nyuki: Mwaka mmoja (1) (NTA – Level 6)

**A. Sifa za Mwombaji:**

**Kozi ya Astashahada ya Awali (Basic Technician Certificate) ya Ufugaji Nyuki**

i. Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne na awe amefaulu na kupata angalau alama D zisizopungua nne (4), kati ya hizo moja iwe ya somo la Biolojia.

**AU**

Mwombaji awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya VETA ngazi ya tatu (NVA Level III) katika taaluma ya ufugaji nyuki kutoka kwenye chuo kinachotambulika na awe amemaliza kidato cha nne

**Kozi ya Astashahada (Technician Certificate) ya Ufugaji Nyuki**

i. Awe amemaliza kidato cha sita na awe amefaulu na kupata angalau alama E isiyopungua moja na S moja katika masomo ya Hisabati, Biolojia, Kemia, Jiografia, Fizikia na Sayansi Kilimo.

**AU**

Mwombaji awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya Astashahada ya Awali (**Basic Technician Certificate**) katika fani ya Ufugaji Nyuki, Misitu, Wanyamapori, Kilimo au Mafunzo ya Astashahada ya Msingi yanayolandana na taaluma ya ufugaji nyuki kutoka kwenye chuo kinachotambulika.

**Kozi ya Stashahada (Ordinary Diploma) ya Ufugaji Nyuki**

i. Mwombaji awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya Astashahada (**Technician Certificate**) katika fani ya Ufugaji Nyuki.

## B. Ada

Waombaji watakaochaguliwa watatakiwa kulipa ada kama ifuatavyo:

i. **Astashahada ya Awali (Basic Technician Certificate), Astashahada (Technician Certificate) na Stashahada (Ordinary Diploma)** Tsh 805,000/=

**Muhimu:**

a. Ada yaweza kulipwa yote kwa awamu moja mwanzo wa mwaka wa masomo au kwa awamu mbili – nusu mwanzo wa muhula wa kwanza na nusu nyingine mwanzo wa muhula wa pili.
b. Ada hiyo haihusishi gharama za chakula, malazi, mafunzo kwa vitendo (field attachment/study tour) na mavazi ya kinga.
c. Nafasi chache za hosteli zinapatikana chuoni kwa gharama ya Sh 270,000/= kwa mwaka inayolipwa kwa awamu moja au mbili.

**ANGALIZO:** Ada zinaweza kubadilika wakati wowote ndani ya kipindi cha mafunzo kadiri itakavyoonekana ni muhimu.

## C. Jinsi ya Kutuma maombi

i. Mwombaji atakeyetuma maombi chuoni atatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo gharama yake ni **Sh 20,000/=**
- Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi vya taaluma pamoja na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay –in Slip) kwa ajili ya fomu.
- Fomu za maombi zinapatikana Chuoni na kwenye Tovuti ya Chuo; **http://www.bti.ac.tz**

ii. Mwombaji atakayetuma maombi kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (CAS) unaoratibiwa na NACTE atatakiwa kufuata maelekezo yanayopatikana kwenye Tovuti ya NACTE; http://www.nacte.go.tz/

## D. Mwisho wa kutuma maombi

Mwisho wa kutuma maombi ni Tarehe **30 Juni 2017**. Aidha, maombi yatakayotumwa baada ya Tarehe iliyotajwa hayatafanyiwa kazi.

**Maombi yote yatumwe kwa:**
Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki,
S.L.P 62,
**TABORA.**
Barua pepe: info@bti.ac.tz

## E. Taarifa kwa watakaochaguliwa.

Majina ya watakaochaguliwa yatatangazwa kwenye tovuti ya Chuo (**www.bti.ac.tz**) na kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (CAS)
Tangazo hili limetolewa na:

**Mkuu wa Chuo, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki**
**Kny: Katibu Mkuu**

**Wizara ya Maliasili na Utalii**